TAASISI YA UTAFIFI WA MIFUGO TANZANIA (TALIRI

Maziwa Faida Tanzania

*Greening the Dairy Value Chain in Tanzania*

*Institutional Relationships and Innovations for Sustainable Milk Production 2021 to 2025*

Lead Partners

Teagasc — Agriculture and Food Development Authority

Supported by

Funded by:

Government of Ireland International Development Programme

Sustainable Food Systems Ireland

# JARIDA MAALUMU LA MAFANIKIO YA

## MRADI WA MAZIWA FAIDA

## 2022/2022 - 2025/2026

• Utafiti • Ubunifu • Teknolojia • Maendeleo



***Miaka 5 ya Mabadiliko Katika Sekta ya Maziwa Tanzania***

**3,000'** Wafugaji walionufaika | **67.4%** Wanawake na Vijana Walionufaika | **54%** Ongezeko la Uzalishaji wa Maziwa | **100 ha** Za Malisho Bora Zimepandwa | **40** Maafisa Ugani Wamewezeshwa Vitenea kazi

@taliritanzania | www.taliri.go.tz | hq@taliri.go.tz

**Maziwa Faida Tanzania**

*Greening the Dairy Value Chain in Tanzania*

*Institutional Relationships and Innovations for Sustainable Milk Production 2021 to 2025*

Lead Partners: Teagasc – Agriculture and Food Development Authority; TALIRI – Utafiti kwa Maendeleo

Supported by

Funded by: Government of Ireland International Development Programme

Sustainable Food Systems Ireland

# YALIYOMO;


1 NENO LA MKURUGENZI MKUU

3 TAHARIRI: MAZIWA FAIDA: KIELELEZO CHA USHIRIKIANO UNAOBADILISHA SEKTA YA MAZIWA TANZANIA

5 RIPOTI YA MRADI WA MAZIWA FAIDA

7 USHIRIKIANO WA TANZANIA NA IRELAND WAENDELEA KUIMARISHA SEKTA YA MAZIWA

8 MRADI WA MAZIWA FAIDA ULIVYOSAIDIA MAGEUZI YA SEKTA YA MAZIWA TANZANIA

11 MALISHO BORA YALIVYOONGEZA UZALISHAJI WA MAZIWA KWA ASILIMIA 54

12 UBORESHAJI WA VINASABA WALETA MATOKEO CHANYA KWA WAFUGAJI WA MAZIWA

13 WANAWAKE NA VIJANA WANAVYONUFAIKA NA MRADI WA MAZIWA FAIDA

14 MASHAMBA DARASA YANAVYOBADILISHA UFUGAJI WA MAZIWA WILAYANI MUHEZA

15 ZIARA ZA MASHAMBANI ZAIMARISHA HUDUMA ZA UGANI KWA WAFUGAJI WA MAZIWA

16 VIKUNDI VYA VITUO VYA KUKUSANYIA MAZIWA (MCC) VYALETA MAPINDUZI KATIKA UTOAJI WA MAARIFA

17 TALIRI YAWEKEZA KATIKA KUJENGA UWEZO WA WATAALAMU WA SEKTA YA MAZIWA

18 MABORESHO YA MIUNDOMBINU NA MAABARA YAIMARISHA TAFITI ZA SEKTA YA MAZIWA

20 USHUHUDA: “MALISHO BORA YAMEONGEZA MAZIWA NA KIPATO CHA FAMILIA YANGU” – BEATRICE ERASTO

22 SHUKRANI KWA WASHIRIKA WA MRADI WA MAZIWA FAIDA

24 SALAMU ZA PONGEZI ZA WANUFAIKA WA MRADI WA MAZIWA FAIDA



# NENO LA MKURUGENZI MKUU WA TAASISI PROF. ERICK KOMBA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Ndugu Wafugaji, Wadau wa Sekta ya Maziwa, Washirika wa Maendeleo na Wasomaji wa Jarida hili, ni furaha kubwa kwangu kuwakaribisha kusoma jarida hili maalum linaloangazia mafanikio, mafunzo na fursa zilizotokana na utekelezaji wa Mradi wa Maziwa Faida nchini Tanzania.

Sekta ya maziwa ni moja ya nguzo muhimu za maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mbali na kuchangia usalama wa chakula na lishe, sekta hii inatoa ajira, kipato na fursa mbalimbali za kiuchumi kwa mamilioni ya Watanzania, hususani wafugaji wadogo ambao ndio wazalishaji wakuu - wa maziwa nchini. Katika azma ya Serikali ya kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 3.1 hadi kufikia lita bilioni 4.3 kwa mwaka, jitihada za pamoja kutoka kwa taasisi za utafiti, elimu, ugani, sekta binafsi na wafugaji ni muhimu sana..

Kupitia ushirikiano kati ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) pamoja na washirika wengine, Mradi wa Maziwa Faida umeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha mnyororo wa thamani wa maziwa nchini.

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huu yanaonesha wazi kuwa uwekezaji katika tafiti, malisho bora, uboreshaji wa vinasaba, huduma za ugani na kujengea uwezo wadau unaweza kuleta mabadiliko makubwa katika uzalishaji na tija ya sekta ya maziwa. Tunajivunia kuona ongezeko la uzalishaji wa maziwa kwa kaya za wafugaji, kuimarika kwa upatikanaji wa malisho bora, kuzalishwa kwa ndama wenye vinasaba bora na kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za ufugaji wa maziwa.

Aidha, mradi huu umeonesha umuhimu wa kuunganisha utafiti na utekelezaji wa vitendo mashambani. Kupitia mashamba darasa, mafunzo, ziara za mashambani na vikundi vya wafugaji, maarifa na teknolojia mpya zimewekwa kuwafikia wafugaji wengi zaidi na kuleta matokeo yanayoonekana katika maisha yao ya kila siku.

Kwa niaba ya TALIRI, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuimarisha diplomasia na ku-

*Inaendelea Ukurasa wa 02..*




Inaendelea ................................

fungua milango ya ushirikiano kati ya Tanzania na mataifa mbalimbali. Juhudi zake zimewezesha upatikanaji wa ufadhili wa Mradi wa Maziwa Faida, ambao umechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya maziwa, ongezeko la tija kwa wafugaji na ustawi wa jamii nchini.

Vilevile, tunathamini sana mchango wa Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania kwa ufadhili wake uliowezesha utekelezaji wa Mradi wa Maziwa Faida. Shukrani zetu pia ziwaendee washirika wote wa maendeleo, taasisi za elimu na utafiti, viongozi wa serikali za mitaa na wafugaji ambao wamekuwa sehemu muhimu ya mafanikio haya.

Tunapoelekea katika hatua zinazofuata za maendeleo ya sekta ya maziwa, TALIRI itaendendelea kuwekeza katika tafiti zenye tija, ubunifu na teknolojia zinazolenga kuongeza uzalishaji, kuboresha kipato cha wafugaji na kujenga sekta ya maziwa yenye ushindani, jumuishi na inayostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hivyo kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Nawahimiza wafugaji wote kuendelea kupokea na kutumia teknolojia zinazotokana na tafiti, kushiriki katika mafunzo na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ili kufikia maendeleo endelevu ya sekta ya maziwa nchini.

Kwa pamoja tunaweza kujenga sekta ya maziwa yenye tija zaidi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**Prof. Erick V Komba**
**Mkurugenzi Mkuu, TALIRI**

# TAHARIRI

## MAZIWA FAIDA: KIELELEZO CHA USHIRIKIANO UNAOBADILISHA SEKTA YA MAZIWA TANZANIA



**Na Martha Julius, Dodoma.**

Sekta ya maziwa nchini Tanzania inaendelea kuwa moja ya sekta muhimu katika kukuza uchumi wa kaya za wafugaji, kuboresha lishe na kuimarisha usalama wa chakula. Pamoja na mchango wake mkubwa, sekta hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa malisho bora, vinasaba duni, athari za mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji mdogo wa huduma za ugani na teknolojia za kisasa.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Mradi wa Maziwa Faida umeibuka kama mfano bora wa namna ushirikiano kati ya taasisi za utafiti, elimu, ugani, serikali na washirika wa maendeleo unavyoweza kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya maziwa. Kupitia Mradi huu, teknolojia na mbinu mbalimbali zinazotokana na tafiti zimefikia wafugaji moja kwa moja na kuleta matokeo yanayoonekana katika uzalishaji na ustawi wa kaya zao.

Jarida hili maalum linaangazia safari ya utekelezaji wa Mradi wa Maziwa Faida kuanzia malengo yake, mbinu zilizotumika, mafanikio yaliyopatikana pamoja na mafunzo muhimu yaliyotokana na utekelezaji wake. Mafanikio yaliyorekodiwa katika maeneo ya uzalishaji wa malisho bora, uboreshaji wa vinasaba, kujengea uwezo wataalamu na wafugaji, pamoja na kuimarisha mifumo ya ugani yanaonesha kuwa uwekezaji katika utafiti wa mifugo una matokeo ya moja kwa moja kwa maendeleo ya sekta.

Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa maelfu ya wafugaji, wengi wao wakiwa wanawake na vijana, wamefikiwa na kunufaika kupitia shughuli mbalimbali za mradi. Ongezeko la uzalishaji wa maziwa mashambani, matumizi ya malisho bora na kuimarika kwa ushirikiano kati ya watafiti, maafisa ugani na wafugaji ni ushahidi wa mafanikio hayo.

Pia, Mradi wa Maziwa Faida umeonesha umuhimu wa kuunganisha tafiti na utekelezaji wa vitendo katika jamii. Kupitia mashamba darasa, ziara za mashambani, vikundi vya wafugaji na mafunzo endelevu, maarifa yameweza kuwafikia walengwa kwa ufanisi zaidi na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili katika mazingira yao halisi.

Tunapoelekea katika hatua mpya za maendeleo ya sekta ya maziwa nchini, ni muhimu kuendeleza ushirikiano huu ili kuhakikisha teknolojia, ubunifu na matokeo ya tafiti vinaendelea kuwafikia wafugaji wengi zaidi. Hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa maziwa, kuimarisha kipato cha kaya, kuongeza ajira kwa vijana na wanawake, pamoja na kujenga sekta ya maziwa yenye ushindani na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Shukrani za kipekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. -

*Inaendelea Ukurasa wa 04 ...*







**Inaendelea ...............................**

Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake wenye maono na juhudi za kuimarisha ushirikiano wa kimataifa. Kupitia diplomasia yake ya maendeleo, Tanzania imefanikiwa kuvutia washirika na ufadhili wa miradi mbalimbali, ikiwemo Mradi wa Maziwa Faida, ambao umeleta matokeo chanya katika maendeleo ya sekta ya maziwa na maisha ya wafugaji nchini.

Pia tunawashukuru wafugaji, watafiti, maafisa ugani, taasisi washirika, Serikali - ya Tanzania, Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wake nchini Tanzania, pamoja na wadau wote waliochangia mafanikio ya Mradi wa Maziwa Faida. Mafanikio haya yanathibitisha kuwa kwa ushirikiano na uwekezaji sahihi katika utafiti na ubunifu, Tanzania inaweza kufikia malengo yake ya maendeleo ya sekta ya maziwa na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wake.

**Martha Julius Nicholaus**
**Mhariri.**



# RIPOTI YA MRADI WA MAZIWA FAIDA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Katika jitihada za kuimarisha sekta ya maziwa nchini Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc), ilitekeleza Mradi wa Maziwa Faida kwa ufadhili wa Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania, huku ikiwashirikisha wadau mbalimbali katika maendeleo ya sekta ya mifugo.

Mradi huu uligharimu Euro milioni 3 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 7 za Kitanzania kwa thamani ya wakati huo, na ulitekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26 katika kata 10 za Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga.

Lengo kuu la Mradi wa Maziwa Faida lilikuwa kuboresha, kuendeleza na kuimarisha mnyororo wa thamani wa maziwa nchini Tanzania, huku ukikabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha ushiriki wa makundi yote ya kijamii, hususan wanawake, vijana na makundi mengine maalum.

Kupitia tafiti zilizofanyika chini ya mradi huu, wataalamu walifanikiwa kutathmini na kupendekeza aina bora za nyasi malisho zinazofaa kwa ng'ombe wa maziwa, hususan aina ya Cenchrus ciliaris, ambayo hustawi vizuri katika maeneo yanayokabiliwa na ukame na mvua chache.

Mojawapo ya mafanikio makubwa ya mradi huu ni upatikanaji na uenezaji wa nyasi hizo za malisho, ambazo zimekuwa suluhisho muhimu kwa wafugaji wanaokabiliwa -

*Inaendelea Ukurasa wa 06..*

## Inaendelea ................................

na changamoto ya upungufu wa malisho, hasa katika kipindi cha kiangazi. Hadi sasa, zaidi ya hekta 100 za malisho hayo zimeanzishwa na TALIRI, wafugaji pamoja na taasisi mbalimbali.

Mradi huu pia umefanikiwa kuboresha mifugo ya maziwa inayofaa na inayostahimili mazingira ya ukanda wa pwani. Aidha, umeongeza uwezo wa wafugaji katika ufugaji wenye tija zaidi, umeimarisha uwezo wa watafiti wa TALIRI kufanya tafiti za kisasa, umeboresha miundombinu na vifaa vya taasisi, na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Vilevile, maafisa ugani 48 walipatiwa mafunzo mbalimbali ya kujengewa uwezo, jambo lililowawezesha kuwahudumia wafugaji kwa ufanisi zaidi. Mradi huu pia umeimarisha ushirikiano wa muda mrefu na mahusiano kati ya Tanzania na Ireland kupitia ushirikiano wa TALIRI na Teagasc.
Sambamba na hayo, Mradi wa Maziwa Faida umechangia utekelezaji wa mipango ya Serikali na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 kupitia Wizara ya - Mifugo na Uvuvi yenye lengo la kuendeleza sekta ya mifugo nchini Tanzania.

Katika kipindi cha utekelezaji wake, Mradi wa Maziwa Faida uliwafikia na kuwanufaisha zaidi ya wafugaji 3,600 wa Wilaya ya Muheza kupitia mbinu mbalimbali za utoaji elimu na uhamasishaji.

Mbinu hizo zilijumuisha mafunzo ya vitendo yaliyotolewa kupitia Chuo cha LITA-Buhuri, programu za mafunzo kwa wafugaji katika jamii zao, ziara za mafunzo ndani na nje ya Tanzania, matumizi ya maafisa ugani wa kata, wakulima na wafugaji vinara, machapisho ya elimu, vyombo vya habari pamoja na mafunzo ya uzamili kwa watafiti.

Leo hii, mafanikio ya mradi yanaonekana wazi katika maisha ya wafugaji. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 50, upatikanaji wa ndama bora umeimarika, na wafugaji wengi sasa wana uhakika wa kupata malisho bora ya mifugo hata wakati wa ukame.

Matokeo haya yamechangia kuongezeka kwa kipato cha kaya, kuboresha lishe za familia na kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.


Tunatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia yanayowezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tunatoa pongezi maalum kwa Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wake nchini Tanzania kwa kufadhili mradi huu muhimu.

Pia tunaishukuru Teagasc kwa ushirikiano wake thabiti katika uhamishaji wa maarifa, teknolojia na utaalamu wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa pamoja na uzalishaji wa malisho bora.

Shukrani zetu za pekee ziwaendee wadau wote walioshiriki kufanikisha utekelezaji wa mradi huu, na zaidi ya yote, wafugaji ambao wamekuwa sehemu muhimu ya mafanikio haya.

Hakika, Mradi wa Maziwa Faida umeonesha kuwa uwekezaji katika utafiti, ubunifu na ushirikiano ndiyo msingi wa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya maziwa nchini Tanzania.

Maziwa Faida — Mkombozi wa Mfugaji wa Maziwa.




**Na Martha Julius, Dodoma.**

Ushirikiano wa muda mrefu kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ireland umeendelea kuzaa matunda kupitia utekelezaji wa Mradi wa Maziwa Faida unaolenga kuimarisha sekta ya maziwa nchini.

Kupitia ufadhili wa Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania, mradi huo umewezesha utekelezaji wa tafiti mbalimbali, mafunzo kwa wafugaji, uboreshaji wa miundombinu ya utafiti na utoaji wa huduma za ugani.

Ushirikiano huo umezikutanisha taasisi mbalimbali ikiwemo Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira na Maliasili (IUCN), Serikali za Mitaa za Wilaya ya Muheza pamoja na wadau wengine wa maendeleo katika lengo la pamoja la kuboresha maisha ya wafugaji wa maziwa.

Katika kipindi cha utekelezaji wake, maelfu ya wafugaji wamefikiwa na kunufaika na teknolojia mpya, mbinu bora za ufugaji na mafunzo yanayolenga kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya maziwa.

Mafanikio yaliyopatikana yanaonesha kuwa ushirikiano wa kimataifa una nafasi muhimu katika kuchochea maendeleo ya sekta ya mifugo na kufanikisha malengo ya Taifa ya kuongeza uzalishaji wa maziwa.

Kadiri Tanzania inavyoendelea kutekeleza mikakati ya maendeleo ya sekta ya mifugo, ushirikiano huu unabaki kuwa mfano bora wa namna taasisi za ndani na washirika wa maendeleo wanavyoweza kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wananchi.

#taliriutafitikwamaendeleo
#UtafitikwaMaziwaZaidi
#MaziwaFaidakwaUfagajiBora



# MRADI WA MAZIWA FAIDA ULIVYOSAIDIA MAGEUZI YA SEKTA YA MAZIWA TANZANIA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Sekta ya maziwa nchini Tanzania inaendelea kushika nafasi muhimu katika kuchangia usalama wa chakula, lishe bora, ajira na kipato kwa wananchi. Hata hivyo, kwa muda mrefu sekta hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji hafifu wa malisho bora, vinasaba visivyo na tija ya kutosha, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA) na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imekuwa ikitekeleza Mradi wa Maziwa Faida tangu mwaka 2021.


Mradi huo unalenga kujenga mnyororo wa thamani wa maziwa ulio jumuishi, wenye ushindani na unaostahimili mabadiliko ya tabianchi. Kupitia utekelezaji wake, zaidi ya wafugaji wadogo 3,000 wa maziwa wamenufaika moja kwa moja na teknolojia, mafunzo na huduma mbalimbali zinazotokana na tafiti.

Mradi umejikita katika maeneo muhimu ikiwemo uzalishaji wa malisho bora, uboreshaji wa vinasaba, kujengea uwezo wadau wa sekta ya maziwa, kuimarisha mifumo ya ugani na kukuza ushirikiano kati ya watafiti, wafugaji na wadau wengine wa maendeleo.

Mafanikio yaliyopatikana yanaonesha kuwa utafiti unaolenga kutatua changamoto za wafugaji unaweza kuwa chachu ya maendeleo ya sekta ya maziwa na kuchangia kufikiwa kwa malengo ya Taifa ya kuongeza uzalishaji wa maziwa.




## VITENDEA KAZI





## MIUNDOMBINU ILIYOBORESHWA NA MRADI






# MALISHO BORA YALIVYOONGEZA UZALISHAJI WA MAZIWA KWA ASILIMIA 54

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Malisho bora ni msingi wa uzalishaji wenye tija katika ufugaji wa maziwa. Kupitia Mradi wa Maziwa Faida, TALIRI imefanya tafiti mbalimbali za kutambua aina za malisho zinazoweza kustahimili mazingira ya Tanzania huku zikiongeza uzalishaji wa maziwa.

Katika majaribio yaliyofanyika, nyasi aina ya Cenchrus ciliaris ilibainika kuwa na matokeo bora zaidi miongoni mwa aina nane za nyasi za malisho zilizojaribiwa. Kutokana na mafanikio hayo aina - hiyo imeanza kuenezwa katika mashamba darasa na kwa wafugaji katika Wilaya ya Muheza.

Matokeo yanaonesha kuwa kaya 40 zilizofuatiliwa kwa karibu ziliongeza uzalishaji wa maziwa kutoka wastani wa lita 5 hadi lita 10 kwa ng'ombe kwa siku. Hii ni sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 54 kutokana na maboresho ya malisho pekee.

Mbali na kuongeza uzalishaji wa maziwa, matumizi ya malisho bora yamechangia kupunguza gharama za uzallishaji, kuboresha afya ya mifugo na kuongeza uwezo wa wafugaji kukabiliana na vipindi vya ukame vinavyotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mafanikio haya yanaonesha umuhimu wa kuwekeza katika tafiti za malisho kama njia mojawapo ya kuongeza tija na ushindani katika sekta ya maziwa nchini.



# UBORESHAJI WA VINASABA WALETA MATOKEO CHANYA KWA WAFUGAJI WA MAZIWA

**Na Martha Julius, Dodoma**

Uboreshaji wa vinasaba umeendelea kuwa eneo muhimu katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini Tanzania. Kupitia Mradi wa Maziwa Faida, wafugaji wamewezeshwa kutumia teknolojia za kisasa za uzalishaji ikiwemo upandikizaji wa mbegu kwa njia ya Uhimilishaji 'Artificial Insemination (AI)'.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa mradi, jumla ya ndama 241 wamezaliwa kwa kutumia shahawa za madume wamezaliwa kwa kutumia shahawa za madume bora ya ng'ombe wa maziwa. Aidha, katika kituo cha utafiti, ndama 107 walizaliwa kwa kutumia shahawa kutoka New Zealand.

Matokeo ya maboresho hayo yameanza kuonekana kwa ongezeko la uzalishaji wa maziwa katika kaya za wafugaji pamoja na kuboresha ubora wa mifugo inayofugwa.

Sambamba na hilo, kanzidata ya mashamba ya maziwa imeboreshwa na mwongozo wa malezi bora ya ndama umeandaliwa ili -umeandaliwa ili kusaidia wafugaji kupata maarifa sahihi ya namna ya kutunza mifugo yenye tija.

***Wataalamu wanaamini kuwa matumizi ya vinasaba bora yataendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza uzalishaji wa maziwa na kuboresha kipato cha wafugaji nchini.***

***#taliriutafitikwamaendeleo***
***#UtafitikwaMaziwaZaidi***



# WANAWAKE NA VIJANA WANAVYONUFAIKA NA MRADI WA MAZIWA FAIDA

**Na Martha Julius, Dodoma**

Mradi wa Maziwa Faida umeweka mkazo mkubwa katika kuhakikisha wanawake na vijana wanashiriki kikamilifu katika maendeleo ya sekta ya maziwa.

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wafugaji zaidi ya 3,000 walionufaika moja kwa moja na programu hiyo, asilimia 67.4 ni wanawake pamoja na vijana. Hali hii imechangia kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji wa maziwa na maamuzi ya kiuchumi ndani ya kaya.

Katika mwaka wa nne wa utekelezaji wa programu pekee, wadau 3,764 walishirikishwa katika shughuli mbalimbali ambapo wanawake walikuwa asilimia 64.7 ya washiriki wote.

Kupitia mafunzo, mashamba darasa, vikundi vya wafugaji na huduma za ugani, wanawake na vijana wameweza kupata maarifa ya kisasa ya ufugaji wa maziwa, kuboresha uzalishaji na kuongeza kipato cha familia zao.

Ushiriki huu unaonesha kuwa maendeleo ya sekta ya maziwa yanaweza kuwa chachu ya uwezeshaji wa kiuchumi kwa makundi mbalimbali ya jamii na kuchangia maendeleo jumuishi nchini.



# MASHAMBA DARASA YANAVYOBADILISHA UFUGAJI WA MAZIWA WILAYANI MUHEZA

**Na Martha Julius, Dodoma**

Mashamba darasa yameendelea kuwa daraja muhimu la kuhamisha teknolojia na matokeo ya tafiti kutoka kwa watafiti kwenda kwa wafugaji wa maziwa.

Kupitia Mradi wa Maziwa Faida, mashamba darasa yameanzishwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Muheza ili kuwapa wafugaji fursa ya kujifunza kwa vitendo kuhusu mbinu bora za ufugaji wa maziwa. Mashamba hayo yanatumika kuonesha matumizi ya malisho bora, mbinu bora za ufugaji wa maziwa.

Mashamba hayo yanatumika kuonesha matumizi ya malisho bora, mbinu za usimamizi wa mifugo, uhifadhi wa malisho na teknolojia nyingine zinazotokana na tafiti za TALIRI na washirika wake.

Mbali na shamba darasa la ekari 50 lililoanzishwa kwa ajili ya kueneza malisho bora, wafugaji wengine wameanzisha mashamba darasa katika maeneo yao na kuwa mfano kwa jamii kuwa mfano kwa jamii zinazowazunguka.

Kupitia mfumo huu wa kujifunza kwa vitendo, wafugaji wengi wameweza kuona matokeo halisi ya teknolojia mpya kabla ya kuziingiza katika mashamba yao, jambo lililochangia kuongezeka kwa kasi ya upokeaji wa ubunifu katika sekta ya maziwa.

Mashamba darasa yanaendelea kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya sekta ya maziwa kwa kuwaunganisha watafiti, maafisa ugani na wafugaji katika lengo la pamoja la kuongeza tija na uzalishaji.



# ZIARA ZA MASHAMBANI ZAIMARISHA HUDUMA ZA UGANI KWA WAFUGAJI WA MAZIWA

**Na Martha Julius, Dodoma**

Moja ya mikakati iliyowezesha mafanikio ya Mradi wa Maziwa Faida ni utekelezaji wa ziara za mashambani zinazowakutanisha watafiti, maafisa ugani na wafugaji wa maziwa katika mazingira yao halisi ya uzalishaji.

Kupitia mradi huo, kaya 40 za wafugaji wa maziwa kutoka kata nane za Wilaya ya Muheza hutembelewa kila mwezi na wataalamu kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya mifugo, kukusanya takwimu za uzalishaji na kutoa ushauri wa kitaalamu

Katika ziara hizo, wafugaji hupata elimu kuhusu malisho bora, afya ya mifugo, uzalishaji wa maziwa, utunzaji wa ndama na mbinu za kukabiliana na changamoto za ufugaji zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, wataalamu hukusanya sampuli za malisho na taarifa mbalimbali zinazosaidia kuimarisha tafiti na kubaini changamoto zinazohitaji ufumbuzi wa haraka.

Mfumo huu umewezesha watafiti kupata mrejesho - wa moja kwa moja kutoka kwa wafugaji na kuhakikisha kuwa teknolojia na ubunifu unaozalishwa unakidhi mahitaji halisi ya sekta ya maziwa.

Kupitia ziara hizo, wafugaji wameongeza uelewa wao kuhusu ufugaji bora na wameweza kuboresha uzalishaji wa maziwa katika kaya zao.






# VIKUNDI VYA VITUO VYA KUKUSANYIA MAZIWA VYALETA MAPINDUZI KATIKA UTOAJI WA MAARIFA KWA WAFUGAJI

**Na Martha Julius, Dodoma**.

Katika kuhakikisha tafiti za sekta ya maziwa zinafanyika kwa ufanisi na kuleta matokeo yanayohitajika, Mradi wa Maziwa Faida umechangia kuboresha miundombinu ya utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI).

Moja ya mafanikio makubwa ni uboreshaji wa maabara ya lishe ya wanyama ambapo vifaa mbalimbali vya kisasa vimeongezwa ili kusaidia uchambuzi wa sampuli za malisho na tafiti ya sekta hiyo.

Mikutano hiyo hutumika kuwasilisha ujumbe maalumu wa kila mwezi kuhusu mbinu bora za ufugaji, kujadili changamoto zinazowakabili wafugaji na kutafuta suluhisho kwa pamoja.

Pia, wafugaji hupata vifaa vya mawasiliano na elimu vinavyowawezesha kuendelea kujifunza hata baada ya mikutano hiyo.

Kwa mujibu wa tathmini za mradi, mfumo huu umeonesha mafanikio makubwa katika kusambaza maarifa kwa haraka na kuongeza ushiriki wa wafugaji katika shughuli za maendeleo ya sekta ya maziwa.

Mafanikio ya vikundi vya MCC yanaonesha umuhimu wa kutumia mifumo iliyopo katika jamii kufikisha huduma za ugani kwa ufanisi zaidi.



# TALIRI YAWEKEZA KATIKA KUJENGA UWEZO WA WATAALAMU WA SEKTA YA MAZIWA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Mafanikio ya sekta ya maziwa yanategemea uwepo wa wataalamu wenye ujuzi na uwezo wa kufanya tafiti zenye matokeo chanya kwa jamii. Kwa kutambua hilo, Mradi wa Maziwa Faida umewekeza kwa kiasi kikubwa katika kujenga uwezo wa wataalamu wa sekta ya mifugo nchini.

Kupitia mradi huo, watumishi nane kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA), wamefadhiliwa kusoma Shahada za Uzamili katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uzalishaji wa maziwa, lishe ya mifugo na maendeleo ya sekta ya mifugo.

Uwekezaji huu unalenga kuongeza idadi ya wataalamu wenye uwezo wa kufanya tafiti za kisasa na kuendeleza ubunifu unaoweza kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji.

Sambamba na hilo, mafunzo mbalimbali yameendelea kutolewa kwa watafiti, maafisa ugani na wadau wengine wa sekta ya maziwa ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wafugaji.

Hatua hii inaweka msingi imara wa kuhakikisha kuwa mafanikio ya Mradi wa Maziwa Faida yanaendelea hata baada ya mradi kukamilika.



# MABORESHO YA MIUNDOMBINU NA MAABARA YAIMARISHA TAFITI ZA SEKTA YA MAZIWA

Na Martha Julius, Dodoma

Katika kuhakikisha tafiti za sekta ya maziwa zinafanyika kwa ufanisi na kuleta matokeo yanayohitajika, Mradi wa Maziwa Faida umechangia kuboresha miundombinu ya utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI).

Moja ya mafanikio makubwa ni uboreshaji wa maabara ya lishe ya wanyama ambapo vifaa mbalimbali vya kisasa vimeongezwa ili kusaidia uchambuzi wa sampuli za malisho na tafiti nyingine zinazohusiana na uzalishaji wa mifugo.

Aidha, huduma za ugani zimeimarishwa kupitia upatikanaji wa pikipiki 10 na gari moja zinavyowezesha wataalamu kuwafikia wafugaji kwa urahisi zaidi - katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi.

Mradi pia umewezesha ukusanyaji wa sampuli bora za malisho na tathmini za mara kwa mara zinazosaidia kuboresha ubora wa tafiti zinazofanyika.

Maboresho haya yameongeza uwezo wa TALIRI katika kuzalisha teknolojia na ubunifu unaolenga kuongeza uzalishaji wa maziwa na kuimarisha sekta ya mifugo nchini.



Malisho Jamii ya Nyasi



Malisho Jamii ya Mikunde



Malisho Jamii ya Miti Malisho



# "MALISHO BORA YAMEONGEZA MAZIWA NA KIPATO CHA FAMILIA YANGU" – USHUHUDA WA MFUGAJI WA MUHEZA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Kwa miaka mingi, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ulikuwa chanzo muhimu cha kipato kwa familia ya Bi. Beatrice Erasto mkazi wa Wilaya ya Muheza, Mkoani Tanga. Hata hivyo, changamoto ya upatikanaji wa malisho bora ilifanya uzalishaji wa maziwa kuwa mdogo na kipato kisichokidhi mahitaji ya familia.

Mambo yalianza kubadilika baada ya kushiriki katika shughuli za Mradi wa Maziwa Faida unaotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula (Teagasc) na wadau wengine wa maendeleo.

Mradi huo unafadhiliwa na Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania ukiwa na lengo la kuboresha mnyororo wa thamani wa ng'ombe wa maziwa.

Kupitia mafunzo, mashamba darasa na ziara za wataalamu mashambani, Bi. Beatrice alipata elimu kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa malisho bora pamoja na mbinu sahihi za kulisha ng'ombe wa maziwa.

"Awali nilikuwa natumia malisho ya kawaida bila kufahamu mahitaji halisi ya mifugo yangu. Baada ya kupata mafunzo kutoka kwa wataalamu wa Maziwa Faida Maziwa Faida, nilianza kupanda malisho bora na kuboresha utunzaji wa ng'ombe wangu. Tofauti imekuwa kubwa sana," anasema Bi. Beatrice.

Bi. Beatrice anaendelea kueleza kabla ya kuanza kutumia teknolojia hizo, ng'ombe wake watatu walikuwa wakitoa wastani wa lita 25 za maziwa kwa siku. Hata hivyo, baada ya kuboresha malisho na kuzingatia ushauri wa wataalamu, -

*Inaendelea Ukurasa wa 21...*




uzalishaji umeongezeka na kufikia wastani wa lita 70 za maziwa kwa siku kutoka kwa kwa ng'ombe wake watatu.

Kwa mujibu wa mfugaji huyo, ongezeko la uzalishaji limechangia kuimarika kwa kipato cha familia yake, kuongeza uwezo wa kugharamia mahitaji ya watoto na kuboresha hali ya maisha kwa ujumla.

"Leo hii napata maziwa mengi zaidi kuliko zamani. Kipato kimeongezeka na nimeweza kuendeleza shughuli nyingine za familia. Mafunzo haya yamenisaidia kuona ufugaji kama biashara yenye tija," anaeleza.

Pamoja na hayo Bi. Beatrice anapongeza mfumo wa mashamba darasa na mikutano ya wafugaji unaotumiwa na Mradi wa Maziwa Faida, akisema umewapa fursa ya kujifunza kwa vitendo na kubadilishana uzoefu na wafugaji wengine.

Anawahamasisha wafugaji wengine kuendelea kupokea na kutumia teknolojia zinazotokana na tafiti ili kuongeza uzalishaji na tija katika shughuli zao za ufugaji.

'Teknolojia hizi zina matokeo halisi. Wafugaji tusisite kujifunza na kufuata ushauri wa wataalmu kwa sababu maend-eleo yetu yanategemea maarifa na ubunifu," anasisitiza.

Ushuhuda huu ni miongoni mwa mifano mingi ya namna Mradi wa Maziwa Faida unavyoendelea kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wafugaji wa maziwa nchini kwa kuwaunganisha na teknolojia, maarifa na mbinu bora za uzalishaji.



# SHUKRANI KWA WASHIRIKA WA MRADI WA MAZIWA FAIDA

Na Martha Julius, Dodoma.

Mafanikio yaliyopatikana kupitia Mradi wa Maziwa Faida yametokana na ushirikiano madhubuti kati ya Serikali, taasisi za utafiti na elimu, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wafugaji wa maziwa wenyewe. Ushirikiano huu umewezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizolenga kuimarisha uzalishaji wa maziwa, kuongeza tija katika ufugaji na kuboresha maisha ya wafugaji nchini Tanzania.

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa uongozi wake, usimamizi wa kisera na mazingira wezeshi yaliyowezesha utekelezaji wa programu hii.

Shukrani za pekee zinatolewa kwa Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania kwa ufadhili wake wa ukarimu na imani yake katika juhudi za kuendeleza sekta ya maziwa nchini. Mchango huu umewezesha utekelezaji wa tafiti, mafunzo, huduma za ugani, uboreshaji wa miundombinu pamoja na shughuli mbalimbali za kujenga uwezo wa wadau wa sekta ya maziwa.

Tunatoa pongezi na shukrani kwa Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc) kwa ushirikiano wa karibu wa kitaalamu, ushauri wa kisayansi na mchango wake mkubwa katika kubuni na kutekeleza shughuli za Programu ya Maziwa Faida.

Aidha, tunazishukuru Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira na Maliasili (IUCN) pamoja na -

*Inaendelea Ukurasa wa 23..*



Inaendelea ................................

UZIKWASA kwa ushirikiano wao katika tafiti, mafunzo, -uhamasishaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi.

Shukrani maalumu ziwaendee viongozi wa Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, maafisa ugani, watafiti, wasindikaji wa maziwa, vyama vya ushirika na wadau wote walioshiriki katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi huu.
Zaidi ya yote, tunawashukuru wafugaji wa maziwa ambao wamekuwa washirika wakuu wa mradi huu kwa kukubali kushiriki katika majaribio, mafunzo, mashamba darasa na shughuli mbalimbali za utafiti. Ushiriki wao umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yaliyopatikana na umewezesha teknolojia na ubunifu uliotokana na tafiti kufikia walengwa na kuleta matokeo chanya katika jamii.

Kwa pamoja, tumeonesha kuwa ushirikiano ni nguzo muhimu ya maendeleo endelevu ya sekta ya maziwa. Tunatarajia kuendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote katika kuimarisha uzalishaji wa maziwa, kuongeza kipato cha wafugaji na kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Asanteni kwa ushirikiano wenu na mchango wenu katika mafanikio ya Mradi wa Maziwa Faida.




# SALAMU ZA PONGEZI ZA WANUFAIKA WA MRADI WA MAZIWA FAIDA

**Na Martha Julius, Dodoma.**

Kwa niaba ya wafugaji na wanufaika wa Mradi wa Maziwa Faida katika Wilaya ya Muheza, tunatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo nchini.

Tunatoa pongezi za kipekee kwa Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wake nchini Tanzania kwa ufadhili wake uliowezesha utekelezaji wa Mradi wa Maziwa Faida, ambao umeleta mabadiliko makubwa katika maisha yetu ya ufugaji, uzalishaji wa maziwa na kipato - cha kaya zetu.

Vilevile, tunatambua kwa heshima kubwa mchango wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti, Ushauri na Mafunzo ya Kilimo na Chakula ya Ireland (Teagasc), kwa kutupatia maarifa, teknolojia na mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa pamoja na uzalishaji wa malisho bora.

Shukrani za pekee zimwendee Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Prof. Erick Komba, kwa uongozi wake imara uliowezesha mafanikio ya mradi katika ngazi ya jamii.

Kupitia mradi huu, tumepata elimu, mbegu bora za malisho, mafunzo ya ufugaji wenye tija, na kuboresha mifugo yetu, hali iliyochangia kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa, kipato na ustawi wa familia zetu.

Kwa moyo wa dhati kabisa, tunatoa shukrani zetu za dhati na kuthibitisha kuwa tutalinda na kuendeleza mafanikio haya kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

***Maziwa Faida — tumaini jipya la mfugaji wa maziwa.***

***"Amesema Bi. Siwema Kihenya, mfugaji na mnufaika wa Mradi wa Maziwa Faida, Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga.***

## Maziwa Faida Tanzania

*Greening the Dairy Value Chain in Tanzania*

*Institutional Relationships and Innovations for Sustainable Milk Production 2021 to 2025*

Funded by: Government of Ireland International Development Programme

Lead Partners: Teagasc Agriculture and Food Development Authority; TALIRI

Supported by: Sustainable Food Systems Ireland

**Mwenyekiti: Dkt. Zabron Nziku**
**Msanifu wa Jarida: Martha Julius**
**Story: Martha Julius**
**Mhariri: Martha Julius**


**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**
**S. L. P 834**
**Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255-0262962377**
**Barua pepe: hq@taliri.go.tz**
**Tovuti: www.taliri.go.tz**

**@taliritanzania**